

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
CHUO CHA UALIMU BUTIMBA
KANUNI NA TARATIBU ZA CHUO**

1.0 UTANGULIZI

Miongozo na taratibu za Mafunzo ya Ualimu zinalenga kuwaanda walimu wenyewe mtazamo, tabia na uelekeo wa taaluma ya Ualimu. Mtazamo, tabia na uelekeo mzuri hujengwa na kukuzwa kutoptaka na matendo mema, na matendo mema huakisi utii wa kanuni na taratibu zinazoongoza. Kanuni na taratibu zifuatazo zitatuwezesha uendeshaji na usimamizi wa mafunzo ya Ualimu kwa kiwango cha juu cha ufanisi na ubora.

2.0 UTII WA SHERIA ZA NCHI NA ALAMA ZA TAIFA

- 2.1 Mwanachuo atawajibika kutii na kuzifua sheria za nchi na alama za Taifa (kama vile bendera ya Taifa, nembo ya Taifa na wimbo wa Taifa).
- 2.2 Mwanachuo hataruhusiwa kwa namna yoyote ile katika mazingira yoyote yale kughushi nyaraka za kiserikali, kielimu, au kiofisi.
- 2.3 Kuenenda kinyume na kanuni 2.1 – 2.2 ni kosa la kinidhamu kwa mujibu wa sheria na kanuni hizi na jinai kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi. Adhabu kwa makosa haya ni kuachishwa mafunzo na pia mwanachuo anaweza kushtakiwa mahakamani.

3.0 HESHIMA NA UTII

- 3.1 Mwanachuo ajiheshimu mwenyewe, awaheshimu wenzake, wafanyakazi na watu wengine anaokutana nao. Salamu itolewe kwa heshima kwa kuzingatia utamaduni na maadili ya Kitanzania.
- 3.2 Mwanachuo awe na lugha yenye hadhi ya taaluma ya Ualimu na matendo yake yaye yanakuza heshima na utu wake. Aidha, lugha zinazoruhusiwa kwa mawasiliano hapa chuoni ni KISWAHILI na KIINGEREZA.
- 3.3 Mwanachuo anapaswa kuheshimu na kufuata RATIBA KUU ya Chuo na shughuli zinazoambatana na ratiba.
- 3.4 Mwanachuo anapaswa kuwa mtiifu kwa kengele au ishara nyingine yoyote itakayomhitaji kufika mahali anapotakiwa.
- 3.5 Mwanachuo sharti awahi wakati wowote anapohitajicha chuoni mfano: kuripoti chuoni, mstarini, bwaloni, ukumbini, darasani, katika kazi za nje na mahali pengine.

- 3.6 Mwanachuo haruhusiwi kujihamisha bweni au chumba alichopangiwa. Aidha kwa namna yoyote ile mwanachuo haruhusiwi kulala bweni ambalo hakupangiwa.
- 3.7 Mwanachuo haruhusiwi kufanya udanganyifu na au upotoshaji wa taarifa wa aina yoyote kwa jambo lolote wakati wote wa mafunzo.
- 3.8 Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni 3.1 – 3.7 atafunguliwa mashtaka ¹na kupewa adhabu ya papo kwa papo ² na kiongozi wa serikali ya wanachuo, mkufunzi au mwadili. Uvunjaji wa kanuni hizi unaojirudia utapelekea mwanachuo kusimamishwa ama kuachishwa mafunzo. Adhabu ya kusimamishwa mafunzo itafuatiwa na kazi ngumu.

4.0 MAHUSIANO

- 4.1: Mwanachuo wa kike haruhusiwi kwenda bweni la wanaume na mwanachuo wa kiume haruhusiwi kwenda bweni la wanawake bila idhini maalum kutoka ofisi ya uadili.
- 4.2: Mahusiano kati ya wanachuo, walezi na jamii yanapaswa kuwa yale ya **Kaka na Kaka, Kaka na Dada, Dada na Dada na Mtoto na Mzazi**. Wanachuo walio kwenye ndoa watoe uthibitisho kwa mwadili na wafuate kanuni na taratibu za chuo.
- 4.3: Mahusiano ya kingono na mtu yeyote hayaruhusiwi.
- 4.4: Mwanachuo anaruhusiwa kutembelewa au kupokea mgeni siku za mwisho wa wiki au sikukuu na sio siku za masomo. Mwanachuo anaelekezwa kuongea na mgeni wake eneo la maduka, na mgahawa (canteen). Wageni wanaruhusiwa kuingia chuoni kuanzia saa 5:00 asubuhi na kuondoka chuoni saa 11.00 jioni.
- 4.5: Mgeni wa dharura wa mwanachuo (atakayekuja chuoni siku za masomo) aelekezwe kwenda ofisi ya Mkuu wa Chuo.
- 4.6: Mgeni wa mwanachuo haruhusiwi kutembelea na kupumzika maeneo ya mabweni (viz. viunga vya bweni na fukwe) pasipo ruhusa kutoka ofisi ya mwadili.

¹ *Mashtaka yatafunguliwa kwa mwanachuo kupewa fomu ya mashtaka yenye orodha ya makosa yake na yeye kutakiwa kijeleza kwa maandishi.*

² *Adhabu ya papo kwa papo inaweza kuwa usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubebe moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kupasua kuni, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua, n.k.*

- 4.7: Mgeni wa mwanachuo haruhusiwi kuingia/kulala katika mabweni ya wanachuo.
- 4.8: Mwanachuo haruhusiwi kwenda nyumbani kwa mkufunzi au mfanyakazi yeote bila ruhusa maalumu. Mwanachuo akihitaji kwenda huko aombe ruhusa kwa Mwadili.
- 4.9: Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni 4.1 – 4.8 atastahili adhabu itakayotolewa na mwadili wa wanachuo na au kamati ya nidhamu. Adhabu zitakazotolewa kwa makosa haya ni pamoja na kusimamishwa mafunzo au kuachishwa mafunzo. Adhabu ya kusimamishwa mafunzo itaambatana na kazi ngumu.

5.0: USAFI NA AFYA : -

- 5.1 : Mwanachuo anaelekezwa kuoga kila siku na kuweka mwili wake katika hali ya usafi wakati wote.
- 5.2: Mwanachuo anatakiwa kuwa na nywele fupi zisizozidi urefu wa sentimeta moja (sm 1) na zinazotunzwa vizuri kwa kuoshwa na kuchanwa. Aidha, wasichana watakaopenda kusuka nywele wanaelekezwa kusuka mtindo wa utii wa roda mistari sita au nane. Kwa watakao bana nywele wanaelekezwa kubana kisogoni kwa kibanio cheusi.
- 5.3 : Mwanachuo haruhusiwi kuwa na kucha ndefu, ndevu na meno yasiyopigwa mswaki.
- 5.4 : Mwanachuo haruhusiwi kupaka rangi za kucha, midomo na kutinda nyusi au kuweka nyusi bandia au kucha bandia.
- 5.5 : Mavazi ya mwanachuo sharti yaye safi na heshima wakati wote.
- 5.6 : Mwanachuo anawajibu wa kuweka matandiko yake na vitu vingine chumbani katika hali ya usafi na unadhifu.
- 5.7: Mwanachuo anawajibika kufanya usafi wa maeneo, bweni, bwalo la chakula, madarasa, kumbi, vyoo n.k. nyakati za asubuhi na siku za mpango kazi. Orodha ya wanachuo (roll call) walio shiriki shughuli za usafi uasubuhi ndizo zitatumika kuandaa chakula cha siku husika. Mwanachuo ambaye hatashiriki usafi atahesabika hayupo chuoni.
- 5.8: Mwanachuo haruhusiwi kuvuta sigara, bangi, kunywa pombe, kujihusisha na dawa za kulevya, ushoga na usagaji.

- 5.9: Wagonjwa wanaelekezwa kwenda zahanati/hospitali kupata ushauri na matibabu. Ruhusa za mapumziko bwenini zitatolewa na mganga, nurse, mwadili au mkufunzi wa zamu.
- 5.10: Mwanachuo atakaye bainika kuwa ana mimba, aliyetoa mimba na anayejaribu kutoa mimba ataondolewa chuoni.
- 5.11: Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni 5.1 – 5.9 atastahili adhabu ya papo kwa papo. Kujirudia kwa makosa kutapelekea mwanachuo kusimamishwa mafunzo na ikilazimu mwanachuo ataachishwa mafunzo.

6.0: MAVAZI:-

- 6.1: Mavazi yatakayovaliwa na mwanachuo wakati wote Chuoni **SHARTI** yawe ya **HESHIMA, SAFI** na yenyewe kuendana na **kanuni za utumishi wa Umma**.
- 6.2: Mwanachuo analazimika kuvalaa sare kamili ya chuo wakati wote na mahali popote (ndani na nje ya chuo) katika kipindi chote cha masomo (semista/muhula) ; isipokuwa wakati wa kazi za nje, nyakati za jioni baada ya masomo, au siku za mapumziko ndani ya chuo.
- 6.3 : Mwanachuo anatakiwa kuvalaa kitambulisho chake shingoni wakati wote awapo chuoni au nje ya chuo kwa lengo la kurahisisha utoaji wa huduma.

SARE KWA WANAUME :

- 6.2.1 Suruali ya buluu nyeusi (darkblue) na nyeusi zenyewe marinda mawili yenyewe mkunjo chini (turn up). Suruali nyeusi itavaliwa siku za jumatatu hadi jumatano na suruali ya buluu nyeusi itavaliwa siku za alhamisi na ijumaa. Aidha, koti la suti lenye rangi sawa na suruali linaweza kuvaliwa. Suruali itavaliwa na mkanda mweusi.
- 6.2.2 Shati liwe buluu bahari (light blue) mikono mirefu
- 6.2.3 Tai ndefu buluu nyeusi (dark blue) na nyeusi. Tai itavaliwa kuendana na rangi ya suruali.
- 6.2.3 Viatu vyeusi vya ngozi vya kutumbukiza (kufunika) kisigino kifupi. Viatu vitavaliwa na soksi ndefu nyeusi.
- 6.2.4 Hairuhusiwi kuvalia suruali chini ya kiuno (mlegezo)

6.2.5 Uvaaji wa jinzi, kaptula, bangili, cheni, vimodo, skafu, makobazi, na pete (zisizo za ndoa) hauruhusiwi.

6.2.6 Mwanachuo anapaswa kuwa na sare ya michezo ambayo ni T- shirt nyeupe na track suit ya buluu bahari. Sare ya michezo ivaliwe tu wakati wa michezo.

SARE KWA WANAWAKE : -

6.2.1 Sketi rinda boksi ya buluu nyeusi (darkblue) na nyeusi zenyen urefu unaozidi magoti na zisizobana. Sketi nyeusi itavaliwa siku za jumatatu hadi jumatano na sketi ya buluu nyeusi itavaliwa za alhamisi na ijumaa. Aidha, koti la suti lenye rangi sawa na rangi ya sketi linaweza kuvaliwa.

6.2.2 Shati iwe light blue mikono mirefu na tai ndefu dark blue na nyeusi. Tai iendane na rangi ya sketi.

6.2.3 Viatu vyeusi vya ngozi vya kutumbukiza kisigino kifupi, na soksi ndefu nyeupe.

6.2.4 Nywele zichanwe au zisukwe mtindo wa utii wa roda mistari mitano hadi nane au kubana kisogoni kwa kibanio cheusi.

6.2.5 Uvaaji wa nguo angavu, khanga, kitenge, suruali, kofia, kilemba, hereni, bangili, mkufu, shanga, pensi, miniskirt, nguo zenyen mpasuo unaozidi magoti, makobazi na pete (isipokuwa pete ya ndoa) hauruhusiwi.

6.2.6 Mwanachuo atakayependa kujisitiri kwa vazi la hijab anaelekezwa kumwona mlezi wake wa kike kwa maelekezo bayana.

6.2.7 Mwanachuo anapaswa kuwa na sare ya michezo ambayo ni T- shirt nyeupe na track suit ya buluu bahari. Sare ya michezo ivaliwe tu wakati wa michezo.

6.4 : Uvaaji wa mavazi yasiyokubalika kwa kuvunja kanuni 6.1 – 6.3 utapelekea mavazi hayo kuchukuliwa na kuhifadhiwa ofisi ya msajili na kufuatiwa na adhabu ya papo kwa papo. Mavazi yaliyoshikiliwa yatarejeshwa kwa mwanachuo atakapomaliza mafunzo.

7.0: RUHUSA:-

7.1: Mwanachuo anapokuwa nje ya mipaka ya chuo ndani ya jiji la Mwanza kwa shughuli binafsi au ofisi, analazimika kuwa na cheti cha ruhusa kutoka kwa mkufunzi wa zamu isipokuwa siku inapotolewa ruhusa ya jumla.

Mwanachuo atakayetoka nje ya chuo bila ruhusa atastahili adhabu ya papo kwa papo itakayotolewa na kiongozi wa serikali ya wanachuo, au mkufunzi. Kujirudia kwa makosa haya kutapelekea mwanachuo kusimamishwa ama kuachishwa mafunzo.

- 7.2: Ruhusa zote za ndani na nje ya jiji la Mwanza zinazopelekea mwanachuo kulala nje ya chuo zitatolewa na Ofisi ya Uadili. Mwanachuo atayelala nje ya chuo bila ruhusa atastahili adhabu itakayotolewa na mlezi wa bweni au mwadili. Kujirudia kwa kosa hili kutapelekea mwanachuo kusimamishwa mafunzo au kuachishwa mafunzo. Adhabu ya kusimamishwa mafunzo itaambatana na kazi ngumu.
- 7.3: Mwanachuo anaelekezwa kutoa taarifa kwa kiongozi wa bweni au mkufunzi wa bweni au mwadili juu ya mwanachuo mwenzake ambaye hayupo chuoni au hakulala chumbani/bwenini bila ruhusa kutoka ofisi ya uadili. Mwanachuo ambaye hatatoa taarifa ya kutokuwepo chuoni au kutokulala chumbani/bwenini kwa mwanachuo mwenzake atahesabika kuwa amekula njama na mwanachuo huyo hivyo atakuwa ametenda kosa sawa na mwanachuo ambaye hayupo chuoni au hakulala chumbani/bwenini.

Aidha, mwanachuo ambaye hatatoa taarifa ya ujio wa mgeni ambaye haruhusiwi chumbani au bwenini atahesabika kutenda kosa sawa na mwanachuo aliyemkaribisha mgeni chumbani au bwenini. Kukaribisha mgeni bwenini au kulala nje ya chuo au kulala bweni asilopangiwa ni kosa lenye uzito wa kusimamishwa au na kuachishwa mafunzo ya Ualimu.

- 7.4: Muda wa mwisho wa mwanachuo kumtembelea mwanachuo mwenzake bwenini wakati wa usiku ni saa nne (4:00) kinyume na hapo mwanachuo atakuwa ametenda kosa linalostahili adhabu ya papo kwa papo.
- 7.5: Ruhusa ya jumla kwa wanachuo hutolewa siku ya **Jumamosi** saa **4.00 Asubuhi (ISIPOKUWA KWA WASABATO ambao ruhusa yao huanza saa 1:00 asubuhi)** hadi saa **11.00** jioni. Siku ya **Jumapili** pamoja na siku za Sikukuu ruhusa kwa wanachuo hutolewa kuanzia saa **1.00** asubuhi hadi saa **11.00** jioni wakiwa wamevaa sare za chuo.
- 7.6: Siku za **Jumamosi**, **Jumapili** na siku za **Sikukuu** ambapo hutolewa ruhusa ya jumla kwa wanachuo kutoka nje ya chuo kutakuwa na **ROLL-CALL³** saa **11.30** jioni ambayo kila mwanachuo lazima ahudhurie. Aidha

³ Mwanachuo atakayekosa kuhudhuria roll call za asubuhi, mwisho wa wiki na siku za sikukuu mara tatu (03) mfululizo atasimamishwa mafunzo. Kujirudia kwa kosa hili kutapelekea kuachishwa mafunzo.

roll call inaweza kuitishwa wakati wowote itakapoonekana inafaa. Adhabu ya papo kwa papo itatolewa kwa kutohudhuria roll call. Kutohudhuria roll call mara tatu mfululizo kutapelekea kusimamishwa mafunzo au kuachishwa mafunzo. Adhabu ya kusimamishwa mafunzo itaambatana na kazi ngumu.

- 7.7: Mwanachuo anapotoka chuoni atumie njia zilizo rasmi (kufuata barabara ya lami au usafiri wa hiace, gari binafsi au bodaboda) na sio kukatiza porini, mlimani, au kupenya kwenye fensi au kupita kwenye makazi ya wafanyakazi wa chuo. Atakayebainika kuenenda kinyume ataadhibiwa papo kwa papo. Uvunjaji wa kanuni hii unaojirudia utapelekea kusimamishwa mafunzo au kuachishwa mafunzo. Adhabu ya kusimamishwa mafunzo itaambatana na kazi ngumu.
- 7.9: Mwanachuo hataruhusiwa kutembelea klubu za pombe, nyumba za starehe na nyumba za **kufikia wageni**. Kukiuka kanuni hii kutapelekea mwanachuo kupewa adhabu. Adhabu zitakazotolewa kwa kosa hili ni pamoja na kusimamishwa masomo kutakakofuatiwa na kazi ngumu au kuachishwa masomo.

8.0: TAALUMA

- 8.1: Mwanachuo anapaswa kuheshimu na kufuata ratiba kuu ya chuo ambayo inaanza saa 11:30 asubuhi na kumalizika saa 5:00 usiku.
- 8.2: Mwanachuo anapaswa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo darasani na vipindi vya muda ziada.
- 8.3: Mwanachuo anawajibika kuwahi na kukaa darasani muda wote wa masomo anaopaswa.
- 8.4: Mwanachuo haruhusiwi kutoroka darasani au kukaa Bwenini kabla ya muda wa masomo kumalizika. Mwanachuo asipokuwa darasani lazima awe Maktaba.
- 8.5: Mwanachuo anatakiwa kushiriki kikamilifu na kuonyesha jitihada katika masomo yote yanayotolewa katika kozi anayosoma na masomo ya ziada, mambo ya msingi hapa ni kuwahi na kuhudhuria darasani, kufanya kazi zote na majaribio yanayotolewa na kufanya mitihani yote (Taratibu za mitihani zitahusika).
- 8.6: Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni 8.1 – 8.5 atastahili adhabu itakayotolewa na mwadili wa wanachuo na au kamati ya nidhamu. Adhabu zitakazotolewa kwa makosa haya ni pamoja

na kusimamishwa mafunzo au kuachishwa mafunzo. Adhabu ya kusimamishwa mafunzo itaambatana na kazi ngumu.

9.0: CHAKULA : -

- 9.1: Mwanachuo atakayeruhusiwa kushiriki chakula cha chuo ni yule tu atakayekuwepo kwenye roll call ya asubuhi na kushiriki shughuli za usafi alizopangiwa. Hatua hii itatuwezesha kufahamu idadi halisi ya wanachuo waliopo chuoni kwa siku husika.
- 9.2 : Milo yote lazima iliwe kwenye Bwalo la chakula isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo. Mwanachuo haruhusiwi kupeleka chakula Bwenini.
- 9.3 : Mwanachuo haruhusiwi kupiga kelele zisizo za lazima wakati wa chakula. Hii ni pamoja na kwenda bwaloni na redio yenyе sauti kubwa.
- 9.4: Mwanachuo haruhusiwi kupika Bwenini au mahali pengine popote pasipo ruhusa.
- 9.5 : Vifaa kama jiko, heater, sufuria, kisu haviruhusiwi chuoni.
- 9.6: Mwanachuo haruhusiwi kumkaribisha mtu ye yote kula chakula cha chuo bila kupewa kibali maalum na Mkuu wa Chuo au mtu anayehusika.
- 9.7: Mwanachuo haruhusiwi kuingia bwaloni na viatu vya wazi (makobazi), kandambilii, kaptula, kanga, vesti, gauni ya kulalia, skafu, taulo, kofia, na vitu vinavyo fanana na hivyo.
- 9.8 : Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni 9.1 – 9.7 atastahili adhabu ya papo kwa papo. Vifaa visivyoruhusiwa vikibainika kuwepo vitataifishwa.

10.0: UTUNZAJI WA MALI YA CHUO : -

- 10.1: Mwanachuo anaelekezwa kutumia mali ya umma kwa kuzingatia dhana ya **uendelevu** na kuepuka gharama zisizo za lazima. Mfano : umeme na mifumo yake, maji na mifumo yake, majengo, vitabu na vifaa vingine vyote. Matumizi na uharibifu wa kizembe wa mali ya umma utagharamiwa na mwanachuo. Matumizi na uharibifu wa kizembe wa mali ya umma wa makusudi utapelekea mhusika kuachishwa mafunzo.

10.2 : Kiongozi wa bweni na wanabweni wana wajibu wa kutunza mali zote za bweni na nyaraka muhimu.

10.2: Mwanachuo haruhusiwi kwa namna yoyote kufanya maunganisho batili ya umeme na maji hatakama yeze ni mjuzi katika eneo hilo. Mwanachuo atakayefanya maunganisho batili ya umeme na maji atasimamishwa au kuachishwa mafunzo.

10.3: Mwanachuo haruhusiwi kuandika maandishi, kuchora au kupaka rangi katika majengo au vifaa mbali mbali pasipo maelekezo maalumu. Adhabu ya papo kwa papo itatolewa kwa mwanachuo ambaye atakaidi.

10.4: Mwanachuo anaelekezwa kurejesha kwa wakati mali ya umma iliyoazimwa. Adhabu ya papo kwa papo itatolewa kwa mwanachuo ambaye atakaidi.

10.5: Wizi wa mali ya umma au mali ya mtu mwingine ni kosa la kinidhamu kwa mujibu wa sheria na kanuni hizi na jinai kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi. Adhabu kwa makosa haya ni kuachishwa mafunzo na pia mwanachuo anaweza kushtakiwa mahakamani.

10.6: Milango ya mabweni (vyumba pamoja na milango mikubwa) ifungwe wakati wa vipindi vya masomo. Viongozi wa mabweni watawajibishwa kwa kutokutekeleza kanuni hii.

10.7: Mwanachuo haruhusiwi kujihusisha na biashara yoyote hapa chuo bila ruhusa kutoka kwa mwadili wa wanachuo.

11.0: HABARI NA MAWASILIANO : -

11.1: Mawasiliano yafanyike kwa kuzingatia daraja la mtu unayewasiliana naye mfano kiongozi, mkufunzi, wafanyakazi wasio wakufunzi, n.k. Lugha ya matusi, kejeli, dharau, dhihaka na za kudhalilisha hazitavumiliwa.

11.2 Mawasiliano yote nje ya chuo ni lazima yafanywe kuitia ofisi ya Mkuu wa Chuo. Hii ni pamoja na mialiko ya michezo, mikutano, semina, warsha baina ya wanachuo na watu au jumuiya ya nje.

11.3 Taarifa ya **msiba, ugonjwa na taarifa nyingine muhimu** kutoka nyumbani zinazomuhusu mwanachuo ziwasilishwe ofisi ya mwandili na mtoa taarifa aliyeo nyumbani.

- 11.4: Wanachuo haruhusiwi kukusanyika au kujaribu kufanya mukutano bila idhini ya Mkuu wa Chuo. Kutenda kinyume na kanuni hii kutapelekea kusimamishwa au kuachishwa mafunzo.
- 11.5: Mwanachuo haruhusiwi kupiga kelele, kufungulia redio au chombo chochote cha muziki kwa sauti ya juu kiasi cha kuleta usumbufu kwa majirani zake.
- 11.6: Mwanachuo au mtu yeote yule haruhusiwi kupiga picha au kurekodi taarifa yeote na kurusha katika vyombo vyahabari na mitandao ya kijamii bila idhini ya mhusika au Mkuu wa Chuo. Aidha izingatiwe kuwa kukiuka maelekezo haya pia ni kukiuka sheria ya makosa ya kimtandao, 2015 na ile ya huduma za habari, 2016.

Kuenenda kinyume na kanuni 11.6 ni kosa la kinidhamu kwa mujibu wa sheria na kanuni hizi na jinai kwa mujibu sheria na taratibu za nchi. Adhabu kwa makosa haya ni kuachishwa mafunzo na pia mwanachuo anaweza kushtakiwa mahakamani.

- 11.7: Matumizi ya simu wakati wa vipindi darasani, kwenye vyumba vyahabari na kwenye mikusanyiko maalumu hayaruhusiwi.
- 11.8 : Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni 11.1 – 11.3, 11.5 & 11.7 atastahili adhabu itakayotolewa na mwadili wa wanachuo na au kamati ya nidhamu. Adhabu zitakazotolewa kwa makosa haya ni pamoja na kusimamishwa mafunzo au kuachishwa mafunzo. Adhabu ya kusimamishwa mafunzo itaambatana na kazi ngumu.

12.0: ULINZI NA USALAMA : -

- 12.1: Mwanachuo anatakiwa kutii tahadhari zote za ulinzi na usalama.
- 12.2: Mwanachuo anatakiwa kutoa taarifa kwa uongozi wa chuo mara tu kunapotokea hali au tukio lisilo la kawaida.
- 12.3: Mwanachuo anawajibu wa kuwa mlinzi wa mali yake binafsi na mali ya umma.
- 12.4: Mwanachuo haruhusiwi kushawishi, kuongoza, kushiriki mgomo na maandamano ya aina yeote bila kibali. Kutenda kinyume na kanuni hii kutapelekea mwanachuo kusimamishwa mafunzo au kuachishwa mafunzo. Adhabu ya kusimamishwa mafunzo itafuatiwa na kazi ngumu.

- 12.5 : Mwanachuo haruhusiwi kumiliki na kuishi na aina yeote ya silaha bwenini. Kuenenda kunyume na kanuni hii kutapelekea mwanachuo husika kusimamishwa au kuachishwa mafunzo.
- 12.6: Mwanachuo atakayebainika kutoa matamshi yanayopelekea tataruki na au chuki na kuhatarisha usalama wake binafsi na au usalama wa wenzake/chuo ataachishwa mafunzo mara moja.
- 12.7 Mwanachuo atakayebainika kugombana na au kuhatarisha usalama wake binafsi na au usalama wa wenzake/chuo ataachishwa mafunzo mara moja.
- 12.7: Kuenenda kinyume na kanuni 12.1 – 12.3 kutapelekea mwanachuo kupewa adhabu ya papo kwa papo.

.....
John Ole Meiludie

MKUU WA CHUO

TAMKO LA MWANACHUO

Mimi..... Tahasusi..... Mkazi.....
nimezisoma kanuni na taratibu za Chuo Cha Ualimu Butimba na kuzitafakari nikiwa na akili zangu timamu. Nategemea kila kilichoelekezwa nitakizingatia kwa HEKIMA NA BUSARA.

SAINI..... Tarehe